

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
Tarehe 29 Desemba 2007**

Waliohudhuria

Ally Saidi Mwishehe
Aseli Wilison
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Izdoly Aludo Kihalule
Juma Ali Salehe Jongo
Kibwana Mohammad Msiga
Paulo Atibu Hatibu
Rahma Ali

Chuo cha Usafirishaji (NIT)

Juma alikutana na Bwana Wemba ijumaa. Bwana Wemba alisema tutapewa barua wiki ijayo ya kutualika kwenye kosi ya usalama barabarani ya tarehe 19. Aliomba orodha ya majina ya watu ambao watahudhuria kosi. Alisema tusizidi watu 50. Tulifanya mswada ya orodha kwa majina ya wao wanaosema watakuja na Juma atamletea.

Guta

Kazi kurekebisha guta imemalizwa wakati wa wiki na guta ilianza kufanya kazi ten alhamisi na Ally Saidi Mwishehe kama dereva mpya. Kutoka wiki ijayo ataanza kuleta Tsh 7,000 kila wiki kwa UWABA.

Ofisi

Elaine alileta dondoo za mkutano wa wiki jana kwenye mkutano huu ili wanachama wapitie, na ataendelea kufanya hivi.

Polisi wa trafiki na sheria za barabara

Elaine alijadili barua kwenda polisi wa trafiki kuomba taarifa kuhusu sheria za barabara na kuomba tukutane na idara ya usalama barabarani. Wanachama wengine walisoma na walisahihisha barua. Juma ataipeleka wiki ijayo.

Paulo alitembelea HUWATA wakati wa wiki kuomba nakala za sheria za barabara na walisema watatafuta na watatujulisha.

Shughuli inayobaki

Kazi ambayo bada haijafanyikiwa: kadi ya kushukuru Bike Nouveau Fabrik (Elaine), kutengeneza taarifa kwa ajili ya ofisi (Elaine), kutengeneza ubao wa tangazo (Ally Saidi Mohammed), kufanya photocopy ya michoro ya Morogoro Road (Ally Saidi Mohammed), kununua helmeti na kutengeneza T-Shirts (Mejah).

Majibu ambayo bado hatujapata: TANROADS, Halmashauri la Jiji, Wamba memorial fund